

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WAMILIKI WA ARDHI AMBAO HAWAJAKUCHUKUA
HATIMILIKI ZAO**

30 Julai ,2024

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatoa taarifa kwa umma kwamba ina zaidi ya Hatimiliki **30,000** ambazo zimekamilika lakini hazijachukuliwa na wamiliki wa ardhi walioomba Hatimiliki hizo kutoka katika Masjala za Ardhi katika Mikoa mbalimbali nchini.

Aidha Hatimiliki hizi zinajumuisha Hatimiliki za kielekitroniki ambazo wamiliki wake wamepewa ujumbe mfupi wa maandishi (sms) kuhusu utayari wa Hatimiliki za maeneo hayo katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

Kutokana na hali hiyo, Wizara inatoa taarifa kwa wamiliki wote wa ardhi nchini ambao waliomba Hatimiliki katika vipindi tofauti na maeneo mbalimbali kwenda kuchukua Hatimiliki zao katika Masjala za Ardhi zilizopo katika maeneo vilipo viwanja/mashamba yao wakiwa na kitambulisho cha NIDA. Aidha, orodha za Hatimiliki zilizokamilika imebandikwa katika mbao za matangazo zilizopo katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Pia, kwa upande mwingine Wizara inaelekeza Halmashauri zote nchini na Ofisi za Ardhi za Mikoa kukamilisha maombi ya Hatimiliki yaliyowasilishwa na wananchi au yaliyokwama kwa sababu mbalimbali ndani ya muda wa wiki moja kuanzia tarehe ya taarifa hii.

Imetolewa na: -

**Katibu Mkuu
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**